JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS

Anwani ya Simu: **"TUME"**
DAR ES SALAAM
Namba ya Simu:2460117
Fax: 255 - 022 – 2460117
e-mail: info@psc.go.tz;
Secretary@psc.go.tz;
Website: ***www.psc.go.tz***

TUME YA UTUMISHI WA UMMA,
JENGO LA UBUNGO PLAZA,
BARABARA YA MOROGORO,
S.L.P. 9143,
DAR ES SALAAM.

RUFAA NA MALALAMIKO YA WATUMISHI WA UMMA YATOLEWA UAMUZI

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Umma, Nyakimura Muhoji amesema Tume katika mkutano wake uliomalizika mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam, imepokea na kushughulikia Rufaa **58** na Malalamiko **30** ya Watumishi wa Umma ambao hawakuridhika na jinsi masuala yao ya kiutumishi yalivyoshughulikiwa na Mamlaka zao za Ajira na Mamlaka za Nidhamu. Muhoji, amesema hayo jana katika mahojiano maalum alipozungumza kuhusu uzingatiaji wa Sheria katika Utumishi wa Umma.

Amesema kuwa, Tume kupitia Mkutano huo ilipokea na kushughulikia jumla ya Rufaa 58 na Malalamiko 30 yaliyowasilishwa mbele yake kwa uamuzi. Kati ya Rufaa 58 zilizojadiliwa, Rufaa 27 zimekataliwa, Rufaa 15 zimekubaliwa bila masharti, Rufaa 10 zimekubaliwa kwa masharti kuwa mashauri yao yakaanze upya kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu. Rufaa 6 zimekataliwa kwa sababu ziliwasilishwa Tume nje ya muda uliowekwa kisheria. Watumishi waliokata Rufaa Tume ni wale ambao, kwa mujibu wa Mamlaka zao za Nidhamu walikuwa wamepatikana na hatia katika makosa mbalimbali waliyotuhumiwa na kusababisha miongoni mwao kufukuzwa kazi.

"Makosa hayo ni pamoja kushindwa kutekeleza majukumu yao; Uzembe; Upotevu wa fedha na kuiingizia Serikali hasara; Utoro (kutofika kazini kwa zaidi ya siku 5 bila ruhusa ya mwajiri); Ulevi na Kukiuka Maadili ya Utumishi wa Umma. Makosa mengine ni watumishi kutokuwa na cheti cha ufaulu wa elimu ya Kidato cha Nne; kuwasilisha vyeti vya kughushi na kutoa taarifa za uongo kwa Waajiri wao (kuonyesha sifa za elimu kuwa ni Kidato cha Nne wakijua kuwa hawana sifa hiyo)", amesema.

Kwa upande wa malalamiko 30 yaliyotolewa uamuzi na Tume, bwana Muhoji amesema kuwa malalamiko 24 yalikubaliwa kwa masharti kuwa yarejeshwe kwa Waajiri yakashughulikiwe upya kwa mujibu wa Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo iliyopo. Malalamiko 4 yalikubaliwa, lalamiko 1 lilikataliwa na lalamiko 1 liliwasilishwa nje ya muda uliowekwa wa kushughulikia malalamiko.

Amefafanua kuwa, wakati wa kupitia Rufaa na Malalamiko yaliyowasilishwa Tume kwa uamuzi, wamebaini udhaifu katika baadhi ya maeneo, kama upungufu katika uandishi

wa Mashtaka na Maelezo ya Mashtaka na hii inatokana aidha na uelewa mdogo wa Mamlaka za Nidhamu au Maafisa wanaosimamia Rasilimali Watu katika kuandaa mashtaka. Hivyo, kunahitajika mafunzo kwa Maafisa Utumishi na kwa Wanasheria. Vile vile, Maafisa hawa wanatakiwa kuwa karibu sana kuwashauri Waajiri na Mamlaka zao za Nidhamu ipasavyo.

Upungufu mwingine ni Kamati za uchunguzi kuundwa na Wajumbe wasiokuwa na sifa; Uchunguzi kutozingatia mashtaka ili ziweze kuyathibitisha au kutoyathibitisha; Kutowapa watuhumiwa haki zao za msingi, yaani kutoa muda wa kutosha, kuwaarifu tarehe, muda na mahali pa mahojiano; kuwapa fursa ya kuhoji mashahidi na mwenendo wa uchunguzi; kuwasilisha taarifa ya uchunguzi nje ya wakati.

"Baadhi ya Mamlaka za Nidhamu zinachelewa kutoa uamuzi na zinatoa adhabu zisizolingana na mashtaka kwa kuchanganya adhabu za makosa mazito na makosa mepesi, na wakati mwingine uamuzi unatolewa na isiyokuwa Mamlaka ya Nidhamu" amesema.

Muhoji amesema kuwa kuna baadhi ya Watumishi wa Umma hawazingatii muda unaotambulika kisheria wa kuwasilisha Rufaa na Malalamiko Tume ya Utumishi wa Umma. Kwa upande wa Waajiri, amesema baadhi yao pia hawazingatii Sheria, Kanuni na Taratibu katika kuhitimisha utumishi wa Watumishi waliohusika katika zoezi la uhakiki wa vyeti.

"Tume inazitaka Mamlaka za Ajira na Nidhamu, Waajiri pamoja na Watumishi kuhakikisha kwamba wanazingatia Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo iliyopo katika kuendesha na kusimamia masuala ya Rasilimali Watu. Waajiri, Mamlaka za Ajira na Nidhamu wanapaswa kusoma, kuzielewa na kuzitumia nyaraka mbalimbali zinazotoa ufafanuzi na maelekezo mbalimbali hususani zinazotolewa na Wizara yenye dhamana na Utumishi wa Umma ili kuboresha maeneo yenye changamoto katika utekelezaji wa Sheria, Kanuni na Taratibu za kiutumishi" amesema.

Kuhusu mafunzo kwa Watumishi wa umma, amesema ni muhimu kwa Viongozi wa Taasisi za Umma kuandaa Mpango wa mafunzo kwa watumishi wao unaotokana na Tathmini ya mahitaji ya mafunzo na wanautekeleza.

Muhoji amesisitiza zaidi kwa watumishi wa Umma kwamba wanapaswa kutambua kuwa jukumu lao kubwa ni kuwatumikia wananchi kwa kuzingatia Maadili ya Utumishi wa Umma na kufanya kazi kwa kuzingatia Sheria, Kanuni, Taratibu na maelekezo halali yanayotolewa na Viongozi pamoja na matumizi sahihi ya taarifa za Serikali.

Imetolewa na:-

KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI
TUME YA UTUMISHI WA UMMA
04 SEPTEMBA, 2019